

Ninampenda
mwalimu wangu.




Ni mwalimu mzuri,
mvumilivu na
mwenye huruma.



Amesuka nywele
zake vizuri.



Ameweka shanga maridadi katika nywele zake.



Shanga zake ni za kijani, nyeupe, nyekundu, na manjano.



Tafadhali mama, nisuke nywele zangu kama vile za mwalimu wangu?



Nitakapokuwa mtu mzima, nitaweka shanga katika nywele zangu.




Nikikua, nitakuwa kama vile mwalimu wangu alivyo!